Naam, kurasa ya arobaini na nne, kuna number five, mwenzangu alisema tutarudia hiyo, na kwa kiswahili, hiyo inaitwa, wacha niwasomee vizuri kwa kiswahili, ndio mfahamu. Inaitwa kanuni ya maadili ya uwongozi na uwaminifu, code of conduct, inaitwa, kanuni ambazo viongozi lazima kufuata. Na nikisomea nyinyi kwa ufupi kwa mfano, inasema, mfanyikazi wa serikali, awezi kupata mishahara mbili, na ya serikali. Inasema kwamba, mfanyikazi wa serikali, anaruhusiwa, kufanya biashara, ama kulima. Na kumbuka kuwa ilikuwa ni commission ya Philip Ndegwa, ambayo iliwaruhusu wafanyikazi wa serikali wafanye biashara na kulima, hapa tumeruhusu. Je, hiyo ni mzuri ama ni mbaya, nyinyi wenyewe mtaamua.

Kitu kingine imesema kwamba, rais na makamu wake, waziri mkuu, na mawaziri wa serikali, permanent secretary, Chief Executive Officers, wale wakubwa wa parastatals, na kadhalika. Pamoja na wajumbe, MPs, awaruhusiwi kuwa na account ya banks, nje ya Kenya.. Halafu, inasema, viongozi wa serikali, au speaker, na naibu wake, lazima watangaze pesa zao, mali yao, wakiwa wanataka kufanya kazi kama speaker, mali yake.

Halafu, mtu yeyote ambaye atachaguliwa kuwa rais, au makamu wake, kabla ya kuanza kazi, lazima atangaze mali yake, na mali yake itaandikwa, kutakuwa na register ya kuandika ametangaza ana pesa gani mwaka huu, kwa hiyo register. Na kila mwaka, atatangaza tena na ikiongezeka, ataeleza vizuri kwamba iliongezeka namna hii. Na kueleza imeongezeka namna gani. Na hiyo register, wakiandika uwongo kwa hiyo register, itakuwa ni hatia, na wanaweza kuhukumiwa kotini.

Viongozi, wanatarajiwa wakiwa ofisi, waheshimu wananchi raia, na hiyo iko kwa hizi kanuni.

Ya mwisho nitasema hapo, ni kwamba, kwa mfano, mtu akienda mahali, na afanye kazi kama tunafanya leo, na apewe zawadi, tuseme nimemfanyia kazi mzuri, hiyo mbuzi sio yake binafsi. Mbuzi, alikuwa anapewa ile mbuzi kwa ajili ya kufanya kazi ya serikali, kwa hivyo atachukuwa mbuzi, na kuchukuwa kwa ofisi na kuacha kwa ofisi, na kadhalika. Nia ya hii, ni kupambana na ufisadi kwa ufupi. Kwa hivyo, tafadhali msome ukurasa arobaini na nne, mpaka arobaini na tano, hiyo nyongesa number five, schedule, kuenda chini. Ndio mwone kama mmekubaliana au la. Kwa katiba ya sasa, hakuna kitu kama hicho.

Kwa ukurasa ya 45, upande wa kulia, ni nyongesa number six. Na hiyo nyongesa, ni ratiba, mipangilio. Vile hayo mabadiliko yote yatatekelezwa, kwa muda gani. Unaweza kusema hiyo maneno ya kanuni, na uwongozi, vitatekelezwa siku gani. Saa ingine inaandikwa miezi sita ingine, wakati wa mwaka moja, kuanzia hii katiba, ingine ni miaka miwili. Yale yote yameandikwa, no time limit, inamaanisha ya kwamba, lazima yatekelezwe kwa miaka mitatu, baada ya hii katiba kukubaliwa, so that is the time frame.

Okay, halafu, kurasa la arobaini na sita, kuna nyongesa number seven, na nyongesa number seven inaitwa powers of national and district governments. Imeelezwe na mwenzangu kwamba, utawala unarudishwa kwa raia, na tumesema kwamba, hasa itarudishwa kwa wilaya, kwa district. Sasa, nyongesa hiyo inasema uwezo wa serikali ya kitaifa ya Nairobi, ni gani, na uwezo wa serikali ya wilaya ni gani. Angalieni, imeandikwa list number one, national government list, ni orodha ya serikali kuu ya Nairobi, itasimamia nini. Kama mkisoma number nine, inasema currency, pesa za taifa. Number eleven inasema prisons, kuhusu jela, na kadhalika.

Halafu list ya pili, inasema uwezo wa serikali ya wilaya ni gani. Tuangalie kwa ufupi number two, local taxes, ama kodi za hapa nyumbani, ama masomo ya nursery, primary, secondary, itasimamia health centers, dispensary, clinic. Itasimamia maji, barabara. Number two, markets and trading centers. Number two, itafanya planning. Number d, agricultural services, land administration, survey, physical planning, trade, licenses na kadhalika.

Haya, katikati ya ukurasa, kuna list ya tatu, inaitwa concurrent list, the concurrent list ni uwezo wa pamoja na serikali ya kitaifa na ya wilaya. Tafadhali someni kwa makini, mjuwe je, uwezo wa serikali ya Nairobi. Tungependa serikali hiyo ya Nairobi, isimamie vile inalipwa hapa haya mambo. Ama hii serikali ya wilaya. Kwa ajili pengine serikali ya wilaya inaweza kupewa uwezo, ifanye kitu, lakini baadaye, mjuwe kwamba, hamna uwezo wa kufanya hiyo kitu, the responsibility, is too heavy msome kwa makini.

Kitu kingine, ningependa kuwakumbusha, kwamba kwa katiba ya mwaka wa sitini na tatu, serikali ilikuwa iko karibu kwa raia. Lakini wakati ule, iliwa serikali ya mikoa, ama ya majimbo, provinces or regions. Wakati huu, hii ni ya district. Orodha ya uwezo, wakati ule ilikuwa imeeleza ya mikoa, ama ya jimbo, na ya serikali ya Nairobi. Wakati huu ni ya district. Pengine mngpenda, kulinganisha tena na ile katiba ya mwaka wa sitini na tatu.

Sasa, katikati ya hiyo page 46, kuna nyongesa number eight, inaitwa transitional and constitutional consequential provisions. Hiyo ni kusema, tukitaka kutekeleza katiba hii mpya, ni mambo gani one lazima yafanywe. Nitasoma ukurasa arobaini na sita mpaka arobaini na saba, lakini nitawasomea kidogo kidogo.

Number two, inaitwa existing Laws. Sheria ambazo ziko sasa, je, ni nini itafanyika? Inasema kwamba, katiba ni sheria kuu. Na, chapter one, inasema sovereignty of the people and the supremacy of the constitution, ukuu wa katiba. Hiyo ni kusema, kama kuna sheria ambazo ziko sasa, na aziambatani na katiba mpya, hizo sheria lazima zibadilishwe, ziambatane na katiba mpya.

Na number three, elections, mkiangalia chini ya hiyo, three, iko number one, two, three, four, mkono wa kulia kabisa, juu. Inasema kwa ufupi kwamba, pengine niwasomee vile imeandikwa. Imesema; mtu ambaye kabla wa mwanzo wa utekelezaji wa katiba hii, amechukuwa madaraka ya rais, mara mbili au zaidi. Mtu ambaye amekuwa rais mara mbili au zaidi, kabla ya hii katiba, ataweza katika katiba mpya, (a), kugombea uchaguzi au kuhudumu kama rais, makamu wa rais, au waziri mkuu. Na,

awezi kuchaguliwa ama kuhudumu kama naibu wa waziri mkuu, ama naibu wa waziri, au mbunge. Anybody ambaye amekuwa rais mara mbili au zaidi, awezi kusimama kama rais, makamu wa rais, prime minister, deputy prime minister, minister, au hata mbunge. Okay?

Haya, ingine, number five, sikizeni, sikizeni number five, kwa mjibu wa kifungo hicho tumesoma saa hii, mtu yeyote ambaye kwa njia nyingine, angestahili kusimama kwa uchaguzi, isipokuwa kwa kanuni za katiba hii, anaweza kusimama kama mgombezi katika uchaguzi wa kwanza utakaofanywa, wakifuata katiba hii, sijui kama mmelewa, nitasoma baadaye. Lakini kwa ufupi, mkitaka kuelewa, mfungue, vile mlielezwa, chapter 8, page 156. Mfungue, tafadhali fungua 156, inasema; mtu anayefaa kuchaguliwa kuwa rais, qualifications for a president. Page 20, katikati hapo, mnaona 156, someni one, yeye lazima awe ni mkenya, si ni kweli?

(b), awe ana umri wa miaka thelathini na mitano, na awe chini ya umri wa miaka sabini.

(c) inasema, mwenye maadhili mema sana, na mwenye sifa njema, asiwe anakosana na wato.

(d) awe na shaada kutoka chuo kikuu, kinacho tambulika. Yaani awe na degree, from a recognized university. Na kadhalika.

Yale tumesema saa hii, na kusema ni nani anastahili kuwa rais wa Kenya. Na kitu kimoja ni kwamba, asiwe chini ya miaka thelatahina na tano, na asipite miaka sabini, na awe na degree. Lakini vile tumeandika, tumesema, lakini wakati huu, ingawa hiyo sharti iko, wale ambao pengine wamepita kidogo, ama hata chini kidogo ya 35, ama hana degree, tutaruhusu wakati huu wasimame. Najua sasa, ngoja kwanza niwasomee, halafu mwishowe tutakuwa na discussion.

Now, chini hapo hapo, kwa hiyo ukurasa, sikilizeni kwa makini, mnaona provincial administration, on page 46, kwa kiswahili inaitwa utawala wa moka. Kwa kingereza, on the coming into the force of this constitution, the system of administration, comprising sub chiefs, chiefs, D.Os, D.Cs, and P.C, commonly known as provincial administration, shall stand dissolved. Inasema, wakati wa kutekeleza katiba hii, mvumo wa utawala unaohojisha naibu wa chief, chief na kadhalika, ambao kwa kawaida inafahamika kama utawala wa mkoa, utafutiliwa mbali. Na hiyo number two inasema, waende public service commission, kutafuta kazi ingine. All those serving under the provincial administration, shall report to the public service commission for re-deployment..

Ingingine, page 47 katikati, imeandikwa, death penalty, and other outlawed offences. Kwa kiswahili imeandikwa, adhabu ya kifo na adhabu nyingine, zilizo aramishwa, zilizopigwa, na Mary amewaeleza kwamba kila mtu ako na haki, na hiyo ya kifungo ya kifo tutafutilia mbali. Sasa kwa kiswahili tunasema, ile uduma ya kifo iliyotolewa na mahakama yoyote, kabla ya utekelezeji wa katiba hii, itaondolewa, na kufanywa kifungo cha maisha. Kwa hivyo kama kuna watu ambao wamehukumiwa kunyongwa, wamekuwa wakisubiri wanangojea kunyongwa, automatically, itakuwa ni kifungo cha maisha.

Na ya pili, tena wanaweza kuendelea kumwomba msamaha. Mnajua kawaida rais ana uwezo wa kusamehe watu, hata hiyo inaweza kupunguza tena.

Na cha pili, in number three there, it says, every sentence of corporal punishment, passed before the coming into force of this constitution, is remitted, and shall not be carried out. Na kiswahili; kila ukumu wa kupigwa viboko, iliyopitishwa kabla ya katiba hii imeondolewa, na haitatekelezwa. Yaani, hiyo maneno ya kusema mtu atapigwa, viboko sijui tatu, ama ishirini, hakuna tena.

Now, niwajulishe, also, mnakumbuka haki ya binadamu, mlielezwa sheria ya haki. Tukirudi Nyuma, legal rights, page 7, upande wa kushoto, inasema, 37 children, muende chini katikati ya page 5, unaona. Every child has a right to, number 5 inasema, kila mtoto ana haki. Na ukiendelea mpaka (g), inasema kila mtoto ana haki, g, kuwa uhuru, kutokana na adhabu ya viboko, ama haina ingine za ukatili, ghasia, na kutendewa kinyama, shuleni, na katika taasisi nyinginezo, zinazoshughulikia huduma za watoto. Kwa hivyo kupiga watoto shuleni kiboko, utakuwa umepiga marufuku, na kadhalika.

Ya mwisho hapo, page 47, mkono wa kulia kabisa kabisa, inasema, past human rights, abuses, niwasomee kwa kiswahili, kukiugaji ya haki za abinadamu, za wakati uliopita. Inasema, tume ya haki za binadamu, na haki za utawala, katika kipindi cha miezi sita, ya kutekeleza hii katiba, kwa malalamiko ya mtu yeyote, au kwa hoja ya tume mwenyewe, (a), itachunguza hali zote za kufika haki za abinadamu, na mtu yeyote, au kundi la watu, kabla ya kuanza kutekelezwa kwa katiba hii. It will investigate, all forms of human rights abuses by any person or groups before this constitution. Itachunguza sababu za migogoro ya kijamii, pamoja na vifo vya halaiki, vita vya kikabila, na kubainisha wale waliohusika. It will investigate the causes of civil strike, including massacres, tribal clashes, and identify those responsible.

(c) Kufanya mapendekezo, yanayofaa kuhusu, to make appropriate recommendations, regarding;

1. The prosecution of those responsible, kuwashtaki wale waliohusika.
2. Malipo ya fidia, kwa walio dhuriwa, the word of compensation to victims.
3. Reconciliation and liberation.
4. Na kuna mwishowe hapo, ni ownership of land, kuna maswala kuhusu ardhi tena hapo.

Now, Mary akawaeleza kwamba chapter 18, ni kuhusu amendment for the constitution, kubadilisha katiba. Niwakumbushe, vile tunasema, kwamba tulipopata uhuru, tulikuwa na hii katiba ya mwaka wa sitini na tatu. Hii katiba ilikuwa na ukurasa mia mbili tisaini na nane, karibu ukurasa mia tatu. Iliandikwa Lancaster House, na wazee, viongozi wa vyama vya siasa, si ni ukweli, akina Ngala, Odinga, Mudiro, Arap Moi, Olei Tipis, Arap Koech, Jeremiah Nyaga, Kikonyo, na wengine, walikuwa kwanza watu kumi na nne, baadaye wakaongezeka wakawa ni watu thelathini na moja, including Maria (?).

Wakaandika katiba ya, karibu page mia tatu.

Kwa hii miaka ya thelathini na tisa ya uhuru, hiyo katiba ikabadilishwa mara thelathini na tisa, karibu mara moja kila mwaka. Mpaka sasa katiba ambayo tunayo, tunarekebisha sasa ndio hii. Ilikuwa namna hii, ikarekebisha, mpaka ikawa hii. Na hii ina ukurasa 98 pages only, ile ingine ilikuwa 298 pages. Taratibu ya kubadilisha, ilikuwa ni kwa bunge, 65% wabunge, wanaweza kubadilisha. Hii ilikuwa na taratibu ya kuibadilisha ambayo ilikuwa ngumu. Kwa mfano kulikuwa na, senate na lower house. Na kubadilisha tungeanzia lower house, na iende tena senate. Lakini hata senate, ikafutiliwa mbali. Ndio ikawa rahisi kuibadilisha hii, hata ikawa namna hii. Sasa, hiyo chapte 18, amendment of the constitution, msome kwa makini, kwa ajili je, mkiwa mmefanya kazi nyingi, vile mmefanya sasa, kuandika hii katiba, halafu mtu mwingine aje abadilishe kila mwaka, atoe moja, moja, moja, mpaka ibaki namna hii, hiyo ni nzuri au la?

Kwa hivyo, kuna taratibu ya kubadilisha, kuna sehemu za katiba, ambazo hazitaweza kubadilishwa bila kuuliza raia, na kuna sehemu zingine zinaweza kubadilishwa, mjue ni gani, msome nyinyi wenyewe.

Nikimaliza sasa, kazi ya mwisho kwa hii, ni swala ya kwamba, je, kuna tofauti gani, kati ya katiba ya sasa, na katiba ambayo tunapendekeza, na mswada, kwa ufupi? Mlijifunza wakati wa civic education, mkajua katiba hii ya sasa sana, ingawa ni ngumu kusoma, na iko tu kwa kingereza, tulikuwa tumefupisha, na kuandika kidogo tu, pocket version, kwa Kingereza na Kiswahili, tuna imani mlisoma kwa makini, na mnajua vile hii katiba iko. Lakini tunasema, hata kama hamjui sana, kwa ajili ni nyinyi mmefinyika ama mmefurahi, waingereza wanasema, the wearere knows where the shoe pinches. Kwa hivyo, for better or worse, this has been katiba ya sasa, tofauti yake na hii ni nini?

Kwanza, tofauti ya hii na hii, tumesema, in fact, kwamba, hata ukiona hii ni kubwa kushinda hii. Je, hii ikichapwa kwa kitabu ya government printer, hata ukiangalia, ni kubwa ama ndogo. Na pengine ikiwa kubwa au ndogo, inategemea vile imeandikwa, pengine itakuwa na mingi zaidi, au chache zaidi, kushinda ile katiba ya sasa.

Kulingana na sura, na chapters, tumesema hii ina how many chapters, 20, Mary read for you upto chapter 20, twenty chapters, inapendekeza chapter ishirini. Hii ina chapter kumi na moja, kwa hivyo hata ukiona kulingana na sura na chapters, utaona kwamba hii has got more than this one. Hii by the way, ilikuwa na 14 chapters, ikarudishwa, mpaka ikawa kumi na moja, sasa hii ina twenty Chapters yani kuna nyongesa.

Kitu cha pili, ni kwamba, hii ina utangulizi, preamble. Mary alianzia utangulizi, preamble. Hii ni kifungua, hakuna utangulizi, there is no preamble, inasema tu one, Kenya is a sovereign republic, okay.

Kitu cha tatu, ni kwamba hii iliandikwa na wazee, ikabadilishwa na wabunge, kuirebisha hii katiba, tulijaribu kuhusisha wananchi, ndio mkisoma, chapter one, ya hii sasa tunapendekeza, inaitwa sovereignty of the people, and the supremacy of the constitution. Kwa Kiswahili sovereignty of the people, inaitwa, uhuru wa wananchi, na uhuru wa katiba. So, wananchi wamehusishwa, kuandika hii, wananchi wamerekebisha wenyewe, kupitia tume, na kupitia conference ambayo intakuwa hivi

karibuni.

Mambo mengine kwa ufupi ni kwamba, kuhusu uraia, kulingana na katiba ambayo iko sasa, mwanaume akienda ngambo, na apate bibi, akija na huyo bibi, huyo bibi na watoto wake watakuwa automatic ni raia wa Kenya. Lakini msichana akienda ng'ambo na apate bwana, na akija hapa, huyo bwana wake awezi kuwa raia wa Kenya, na watoto hawawezi kuwa raia wa Kenya, bila kuapply wakiwa miaka zaidi ya kumi na nane.

Sasa, hii katiba kwa ufupi, inajaribu kusawalisha wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, wazee na akina mama, kwa ufupi. Kuna njia nyingi, zimeandikwa kwa hiyo chapte inaitwa, bill of rights, chapter five, someni kwa makini, inasema mwanaume na mwanamke ni sawa. Lakini tena inaangalia kwamba wanawake wameteswa miaka nyingi. Tena tukasema, 30% ya viti bunge, ni ya wanawake, mtoto msichana na mvulana wana haki sawa ya kuridhi mali kwa wazazi. Mwanaume, yaani baba ya mtoto na mama ya mtoto, ikiwa wameowana ama wajaowana, lazima watunze huyo mtoto, na kadhalika, okay?

So, kwa hivyo, ningependa msome kwa makini, mjue hiyo chapter, kuhusu equality of sexes or gender, ethics and quality. Kitu ingine, ni kwamba, mkisoma hiyo bill of rights, kuna haki nyingi zimeandikwa, haki na masomo ya kimsingi, na ya secondary, haki kuwa na mahali pa kuishi, haki ya kuwa na chakula, haki kuwa na matibabu, na kadhalika. Ni nyingi kushinda zile ziko hapa, lakini, tumesema, sio tu kuandika kwa karatasi, serikali lazima itekeleze, itimize, haki hizo. Na kama serikali inasema pesa hakuna, lazima ieleze kwa ajili gani pesa hakuna. Kitu cha pili, ni kusema pesa itapatikana lini, na iwe na mipangilio ya kutekeleza, a program for the provision of those basic rights.

Kwa hii katiba mpya, inapendekeza Nyumba mbili za bunge, mnajua wakati wa uhuru, vile tumesema kulikuwa na senate na lower house, sasa tunapendekeza kutakuwa na national council, vile mmelezwa, na national assembly, Nyumba mbili za bunbe. Je, mnapenda Nyumba mbili au moja. Na ile ya pili, iwe inafanya nini, tafadhali someni.

Kwa jumla, bunge itakuwa na nguvu zaidi, kulingana na hii katiba, hata maneno ya kuhusu bunge tumeandika mbele, chapter 7, the legislature. Tumetangulia kusema maneno ya the legislature, halafu chapter 8, ni executive, ni kweli? Kwanza tumesema maneno ya bunge, halafu ya serikali yenyewe. Kwa katiba ya sasa, ukisoma, ni opposite. Chapter 2, ni executive, na chapter 3 ni parliament. Parliament itakuwa na nguvu zaidi kwa ufupi.

Naam, kulingana na maneno ya parliament, tutakuwa na njia mbili ya kupiga kura, wakati huu, ukipigia kura MP, kuna njia moja tu, kama watu wa KANU wanasimama, yule atapata kura zaidi, anakuwa MP, si ni kweli? Lakini sasa, tumependekeza tena kuongezwe njia ingine, utakuwa unapigia MP, halafu upige tena ya party, tumesikiza kwamba kutakuwa na viti tisaini, 90 extra seats, those are called party lists. Pengine mtatakata kujadiliana, inamaanisha maybe you can not say what are the 90 seats for, unapigia MP na unapigia chama, sio kama sasa.

Halafu, mtu anaweza kusimama, akiwa hana chama, kuwa MP ama kuwa rais, na kadhalika, ama vice president. Sio kama sasa ambapo unajua watu wengine walishindwa kwa vyama vyao wakaenda kwa chama cha Harun Mwau, ambayo inaitwa Party of the Independent candidates of Kenya, hiyo ni kusema, chama cha wale ambao hawana chama. Lakini sasa, kutakuwa na mtu kabisa ambaye hana chama chochote anaweza simama.

Vyama vy siasa, vimeandikwa ndani ya hii katiba mpya, kwa hii ya zamani hakuna kitu kuhusu vyama vya siasa, na tunajua kwamba, ya kuregister chama cha siasa, imekuwa ikifanywa na registrar of societies. Sasa, vyama vitakuwa vinaruhusiwa na electoral commission of Kenya. Na chama hili kiandikishwe, lazima ifuate kanuni za democrasia ndani yake, wapige kura regularly and so on. There are rules internal for a party. Na kama chama kitapata zaidi ya 5% ya kura zote, kitapewa pesa za serikali kiasi kidogo ya kufanyia kazi ya chama. Kwa hivyo tutakuwa na political parties funds.

Wajumbe hawataweza tena, kuamua swala la mishahara yao. kutakuwa na ile salaries and remuneration commission. Unaweza kama mjumbe anapotelea Nairobi ama sehemu zingine, anaweza kurecall, kuna kitu ya kuweza kufuta yeye kabla ya miaka mitano kuisha.

Lazima hao viongozi wote, wa sign ile kanuni, ile tulisoma, na wakati huu, hakuna ile kanuni.

Now, kuchaguwa rais kutabadilika kidogo, wakati huu ni 25% Mkoa tano as simple majority. Sasa tumependekeza kwamba, rais lazima awe na kura 50%, hamsini kwa mia, na apate 20% na kwa mikoa mitano. Ikikosekama mtu mmoja wa kushinda namna hivyo, sasa yule number one na number two peke yao, watapigiwa kura tena, kwa muda wa wiki tatu, na yule atashinda tu, ndio atakuwa rais. Kwa ufupi, rais, uwezo wa rais unapunguzwa, ya bunge inaenda juu. Rais atakuwa, uwezo wake unapunguzwa chini, na ile instrument yao, inaitwa Provincial Administration, wamekuwa wanatumia saa hii itafutiliwa mbali.

Haya, kutakuwa na waziri mkuu, na kwa hii katiba hakuna waziri mkuu.

Ministers, vile tumeelezwa, hawatakuwa wajumbe, wabunge. Kwanza tumesema, ministries ziwe kumi na tano tu. Lakini tena, minister au naibu hawawezi kuwa wajumbe wa bunge. Tumesema wengi, wanapenda kusema ninaenda bunge, nitaleta bendera sehemu yetu, hiyo bendera itapotea. Kwa ajili tukasema, kwamba hao ministers, ukiuliza kwa ajili gani aji constituency, anasema nilikuwa nafanya kazi ya taifa Kwale, sasa atakuwa tu mbunge wa hapa na kurudi nyumbani, na kama hatakuwa narudi sana, anaweza kufutwa. Yaani, ministers wawe kama wamerika, ambao si wajumbe wa bunge.

President can be impeached, akifanya makosa.

Minister anaweza kupoteza kiti chake, through vote of no confidence.

Kutakuwa na hiyo serikali ya kukaribi raia, kwa hii katiba sasa, hakuna, lakini ilikuwa kwa ile ya kwanza. Lakini ile ya kwanza ilikuwa ya province, na wakati huu ni ya districts.

Halafu kutakuwa na supreme court. Koti kuu ya sasa ni High Court, halafu kufuatwa na Court of appeal. Lakini kutakuwa na supreme court, ambayo itakuwa inashughulikia wakati mwingine, maswala ya kikatiba.

Koti ya waislamu ya kadhi, imeongezewa.

Halafu administration police, AP, watafutwa hata wao, kwa ajili wao ni watu wa provincial administration. Lakini vile tumependekeza ni kwamba, wa join the regular police.

Na police wameandikishwa kwa katiba, na jeshi, na security forces, hata intelgency, wameandikiwa kwa hii katiba. Kwa hii kulingana na hii ya zamani, hakuna kitu kuhusu majeshi. Halafu, kuna maswala mengine, ambayo yalikuwa hakuna kwa ya kwanza, kuhusu mazingara, haki za watu ambao wanaweza kuthuriwa, haki za watoto na wanawake na kadhalika, what we call emerging constitutional issues.

Sasa nikimaliza kabisa, ni kwamba, haya yote tunayafanya, tukiwa tunajitayarisha kuenda kwa mkutano mkuu wa kitaifa, wa marekebisha ya katiba. Kwa gazeti ya leo, the Daily Nation, ukuraza ya ishirini mpaka ishirini na mbili, kuna list ya delegates ambao wataenda mkutano. Arap Korir, alikuwa amesema mkutano unaanza tarehe ishirini na nane, lakini mawakilishi wanatakiwa wafike tarehe ishirini na mbili, hiyo ni Wednesday next week. Kwa hivyo imebaki one week.

Orodha ya mawakilishi nitasoma, ni watu mia sita, ishirini na nane, kwanza watakuweco wajumbe wote wabunge, hao ni watu mia mbili ishirini na tatu, all the MPs. Halafu kutakuwa na mwakilishi mmoja, kila chama tutakuwa na mwakilishi mmoja, chama cha siasa, vyama arobaini na moja, ambavyo vilikuwa vimeregisteriwa mwaka wa elfu mbili, October tukianza kazi ya kurekebisha katiba, hao ni watu arobaini na moja. Halafu kila district itakuwa na wakilishi watatu. Wa Kericho, mlikuwa mmesomewa, it says, Christine Cheron Ng'eno, Joseph Maritim Soi, na James Kirui Kosgei, hawa watatu. District ni sabini, kwa hivyo ni watu mia mbili na kumi. Halafu, kutakuwa na watu wa civic society. Watu wa vyama vya wafanyikazi, professional associations and organizations, na vikundi vya akina mama, religious organization, dini na kanisa, na watu wengine tunaita special interest groups. Hao ni watu wengine mia moja ishirini na sita, na commissioners, 29 watakuweco, lakini wao hawapigi kura kwa mkutano. Kwa ajili, kura itakuwa inapigiwa ile katiba ile sisi wenyewe tumependekeza. Kwa hivyo tutakuwa kama observers or consultants. Ndio hawa watu sasa mia sita, mia tano tisaini na tisa, au mia sita tuseme. Ndio wataamua kuhusu katiba. Na wanatakikana wakubaliane kwa kauli moja, by consensus. Na wakikosa kusikilizana, kutakuwa na kupiga kura.

Kwa maswala ya sio ya kikatiba, tuseme kwa mfano, chapter tatu, iwe chapte mbili ama chapte nne, pengine kubadilisha vile imepangwa, itatakiwa simple majority, 301 from 600.

Lakini swala la kikatiba, ni kama mtu asema, tuondoe kabisa ile chapte number 11 kuhusu land, tutoe kabisa, ama tuingize ingine ambayo haiko hapa, hiyo ni swala ya katiba, na itapatiwa watu mia nne, kati ya mia sita, two thirds majority. Sasa kitu cha kwanza, you have one week, kujadiliana, muelewe kila kifungo, kwa ajili nyinyi Ainamoi, Kericho, pengine kuna maswala ya muhimu kweli kushinda zingine, mkubaliane, mpe delegates instructions, vile ataenda na kusema, na kupiga kura. Hao sio watu ambao wanaenda na maoni yao pia ya binafsi, wanaenda kuwawakilisha nyinyi, si ni kweli? So you must check. But at the same time, msicheck tu vile mnafikiria, kwa ajili watu wenu ni watatu wa Kericho district, na MPs watatu, kwa ajili kuna constituencies tatu, hiyo ni watu sita. Na simple majority ni 301, and two thirds majority ni 400. Je, how do you multiply 6, mpaka ifike 301, mpaka ifike 400. So, you must also know, wanasema nini wale watu wa (?) and then, mnalinganisha na maoni yenu. Halafu, wakienda kwa mkutano wanatakiwa wafanye lobbying, networking, si ni kweli? Kujadiliana na watu.

Sasa kwa mfano, na hiyo ni ya mwisho, kwa mfano watu wengine wametuuliza tukiwa sehemu zingine hapa, kwamba, hii maneno ya waislamu imezidi sana, why do you have the kadhis court very strong. Tukasema lakini waislamu wamependekeza namna hii. Lakini ukiuliza wewe mwenyewe, kwani inakuhusu kwa njia gani? Kama waislamu wamesema wanataka kuowa bibi nne, na kuwapiga talaka the same day, kwa ajili wewe sio muislamu, why are you bothered. Lakini waislamu watataka nini, kusaidiwa kupitisha hiyo. Sasa pengine inakuudhi wewe chapter eleven, ambayo inahusu ardhi, na pengine watu wa North Eastern, hawana problem ya ardhi, kwa ajili hakuna ardhi, si ni ukweli, kuna tu mchanga. Sasa mnaweza kuuleza, tafadhali nyinyi mtupigie kura, kwa hii sehemu kuhusu ardhi, na sisi pia tutawapigia, ikifika hiyo maneno ya kuowa bibi nne, kulingana na ni sawa.

Kwa ufupi, kazi ndio hiyo tulikuwa tunatakiwa kuifanya, tunasema tu tanawatakia kila raheli, katika uundaji wa katiba, vile chairman wetu alisema. Happy constitution making. Jukumu sasa ni lenu, commission imefanya kazi yake, tutakuwa observers, halafu tueleke sisi wote nyumbani, hayo yote yakiisha.

Caroline Korir: Haya, kabla tujaenda kwa discussion, ningependa kuwajulisha kwa delegates ambao mmechaguwa, mnatakikana muwaone, halafu mjuwe kama ni watu wenu ama walitoka nje. Delegates hebu simama niwatambulishie kwa wananchi. Muone mbele hapa, mnaweza kuja mbele hapa.

Christine Ng'eno: Kwa majina naitwa Christine Ng'eno, natoka katika location ya Soi, Ainamoi Division

Joseph Arap Soi: Mimi ni Diwani Joseph Arap Soi, from Kipsigis County Council, natoka sehemu ya Kipkelion, Kibeneti, huko.

Christine Ng'eno: Okay, wako watatu, mko na hawa wawili, halafu watatu anaitwa Dr. James Kosgei, ambaye ni lecture

Kenyatta University, angeweza kuwa na sisi siku ya leo, lakini wataenda Nairobi 22nd for a seminar, in preparation for the conference. Lakini nafikiri wale ambao wanatoka pale Sosiot, mnamjua Dr. James Kosgey. I think we will go for discussion, ama mnaweza kutoa maswali mko nayo kwa commissioner, halafu atawajibu baadaye. Kama kuna maswali ama comments yoyote, mnaweza kutoa.

Mnaweza karibia hapa, ndio tunase.

Thomas Leting’: Commissioners, jina langu ni Thomas Leting’. Nina swali kuhusu proposals zenu commissioners, kwamba, Dunia hii tuko na system mbili, ya utawala. Moja Military system, pili, Royal system, sijui ni gani mnafuata kwa hii yenu.

Kitu ingine ambayo ilionekana kwa hii proposal zenu, ambayo wengi wetu tulitoa, ni kuhusu white islands, mashamba ambayo yalinyakuliwa kutoka kwa mwafrika, 1901 - 1911. Halafu wazungu wakapewa, ilinyakuliwa kutoka kwa wenyewe. Na wakati tulipaka uhuru, constitution hiyo ya kwanza, ilikuwa inarecognise hiyo, ile ulionyesha sisi. Constitution ya pili, ndio ilitowa. Na lease ya yale mashamba, itakwisha the year 2004, na hatuelewe haya mashamba, imerudishwa kwa wale wenyeji wenyewe, ama imeenda kwa watu gani. Hiyo ndio swali tulisema lazima lichunguzwe na commission.

Kitu ingine, ambayo tulipropose, ambayo sioni kwa hiyo proposal zenu, ni kwamba, kuna sheria ya kienyeji, ambayo tunaita customary law, na hatuioni kwa hii proposal zenu, na hiyo ni lazima, kwa sababu hiyo inatawala wenyewe, kama ni kabila la Kipsigis, tuna namna tulikuwa tukijitawala, tuna sheria zetu tulikuwa tukizifuata. Na ni la zima, hizo sheria haziwezi kutupwa mbali na mtu tu yeyote. Nafikiri nimeeleweka hapo.

Kitu ingine niliona mlikubaliana nayo, kwa proposal zenu, ni civil servants kuwa na business. Hiyo kwa maoni yangu sioni kama ni vizuri, hiyo italeta magendo zaidi. Ile commission ya Ndegwa commission, ndio ilifanya nchi hii kuwa corrupt zaidi. Na ingefutiliwa mbali, civil servants, kama ana shamba yake alime, na mshahara yake tu, asifanye biashara. Biashara, ataingiza kwa ile kazui yake, atakuwa ni magendo magendo, namna tunajua sasa. Alime shamba lake na mshahara yake.

Inginge mlipropose ambayo naoni ni mzuri, lakini sijui kama itawezekana. 30% of women representation, tuseme kama Ainamoi hapa hakuna mwanamke hapa amejitokeza kutaka parliament, tutafanya nini? Kama hakuna mmoja amejitokeza tumfuate kando, tutafanya nini, tupate hii percentage?

Inginge, hii nomination ya parliament, 90, ni ya nini hao watu wote. they are about half of the elected representative, na hao ndio wataleta uchochezi kwa parliament, na senate. Ya nini hao watu wote, I mean, if we have 210 for instance right now, to add another 90, si hii parliament itakuwa haina kazi. Let us have 30% and most of them be women. Kama mnataka wanawake wawe represented properly.

Nafikiri, commissioner, nafikiri hayo, kama unaweza kujibu zingine hapa, kama hamwezi kujibu, myapeleke, asante.

Charles Kipruto Arap Ng'eno: Okay asante sana commissioners, langu ni kuhusu, jina langu ni Charles Kipruto Arap Ng'eno. Langu ni kuhusu watoto. Rights of children

Tumesikia ya kwamba, watoto hawapaswi, labda kupigwa shuleni. Na swali langu ni kwamba, na nyumbani je, wazazi wana haki ya kuchapa watoto ama la? Na ikiwa hivyo, bibilia inasema, ukiweka kando kiboko, ndio unaharibu mtoto. Sasa sijui sheria hii, inaenda kuharibu watoto, ama inaenda kusulihisha.

Lingine la pili, vile tumejifunza wakati huu, sijawai kusikia jinsi corruption itakapoweza kuepukwa. Sana sana, tunapotembea barabarani, tunaona polisi wanashika pesa ana kwa ana. Tuseme ukiwa matatu, unaona anapewa pesa ndio anaondoka. Sijui juhudi itafanya namna gani katika katiba hii, ikomeshe mambo kama hayo, ama mambo ya kupeana rushwa, katika ofisi. Kwa sababu tunaona, umasikini uliotutawala wakati huu, ni kuhusiana na corruption.

Jambo lingine, ni kuhusiana na strike, kama wakati huu walimu wameenda kwa strike, na inaonekana sijui kwa katiba inaweza kusuluhisha aje, hili watoto wa nchi hii, waweze kuendelea na right to education. Na ile pesa walimu wangekula wakati walipoanza kukoma, zitaenda wapi?

Tena katika katiba hii, mambo ya masomo kama 8:4:4 ama ile ilikuwa ya 7:4:2:3, sijui gani ilipendekezwa.

Mambo ya land, sijui kila citizen, yaani mwenyeji wa Kenya, atapaswa kuwa na ardhi, au wengine watakuwa na ardhi, na wengine wasiwemo.

Kwa hayo machache nakomesha maswali yangu, asanteni sana.

Isaak Kosgei: My names ar Isaak Kosgei, and I have been looking at the implementation list for the district, on page 46. I have seen that, among the functions to be performed at the district level, it shall include the use of local taxes, maybe to finance, education services, nursery, primary, and secondary education, and I have seen the the bill saying that it will also finance medical and helath services. I am worried because, it is possible that certain districts may not be able to raise enough funds, to finance the implementation of their development plans.

And, like for example, the nursery schools are now being financed at the district level, and most of them have become non functional. So, if we are now extending to primary and secondary, I am worried things might be bad.

I also know that, the medical services at the district, may not have been fully financed, even by the central government. Now that we are saying, every district is going to look into the medical services, what happens even for such areas, like we said North Eastern, where they may not raise enough funds, to finance this services.

Another observation that I have made, is in connection with the Teachers Service Commission. I have seen the functions of the Teachers Service Commission, does not include remuneration of those teachers. When I went to salaries, and remunerations commission saw that it is only concerned, with the remuneration of I don't know constitutional offices, and I wonder in the whole constitution, I think the Teachers Service Commission, was also supposed to remunerate teachers. Is it because it is going to the district, or what is happening? Thank you.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Kainenyun ko Kipkosgei arap Chepkwony.*

Translator: Jina lake ni Kipkosgei Arap Chepkwony.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Kamache amwa ale kagibarwech mpakaisiek ab Uganda, Tanzania ak Ethiopia,*

Translator: Tumeonyeshwa mipaka za Uganda, Ethiopia na kuinginepo.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Oko tomkibarwech che ba province ne nyon.*

Translator: Na zile za province hatujaonyeshwa.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Amun che ba province,*

Translator: Kwa sababu zile za province,

Kipkosgei Arap Chepkwony: *koribe bariosaiek en mpakait ne kigagikachi kutusaik Mungu.*

Translator: Inatunza hali ya kutoelewa kati ya makabila, vile ambavyo ilikuwa imepangwa hapo awali.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Ne ngot ko makichob*

Translator: Ambavyo, isipotengenezwa,

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Ko tugergetu ak ne ba Israeliek ak Palestiniek*

Translator: Inaweza kuwa kama ile ya wa Israeli na wa Palestina.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Amun mache chitage kobut ng'atutik, amun ye ng'alal en yu,*

Translator: Maana mwingine huuenda anataka kuvunja zile sheria ambazo, maneno ambayo tumepanga hapa.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Ak ole kimenye olantugul.*

Translator: Na kusema mtu haishi mahali popote.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Mayan ng'aliondonono*

Translator: Sikufurahia neno lile.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ng'aliot ake Bwana commissioner,*

Translator: Neno la pili Bw. Commissioner,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Kele chito ne kabaris,*

Translator: Imesemekana kwamba labda yule mtu ambaye ameuwa mwenzake,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko magebare.*

Translator: Naye awezi kuuwawa,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Mayan ng'aliondonono.*

Translator: Sijafurahia neno hilo.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Amun barisie chito inguni ak kole anawe Serikali, aitu karon*

Translator: Maana mtu huenda, anaweza kusema nikuuwa leo nitapelekwa na kesho tena nitarudi.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko ngot kagitiach kele ma kebare, kotiana bik che begu.*

Translator: Ikiwa basi mmesema hakuna kuuwa wauwaji, watu wangapi wanaweza kuuwawa?

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Mayan ng'aliondonono.*

Translator: Haikunifurahisha.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ng'aliot ake,*

Translator: Neno lingine,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko kage mwa ng'alek ab corruption.*

Translator: Hayo maneno ya ufisadi yameshatajwa,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Labda hekari kumi, ingine ishirini,*

Translator: Vile amesema

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ak age artam,*

Translator: Mwingine arobaini,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko age ne matinye chorwet, ne maingen chi kigachin oeng ak nusu.*

Translator: Yule ambaye hana rafiki, na ajulikani na mtu, uenda akapewa hekari mbili na nusu,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko nikamwa ale imanit ab serikali ko mi yebano en yoton.*

Translator: Kwa hivyo nimeuliza kwamba, je, haki ya serikali iko wapi?

Kipkosgei Arap Chepkwony:*A ngen ale serikali ko uniform tuguk che chik.*

Translator: Najua serikali inahitajika kuwa na mambo yake, kuwa uniform sawa kwa watu wote.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ingogerwech corruption ne ba imbarenichon kogikaito che ba serikali.*

Translator: Ituangalilie, corruption ambaye iltekelea ufisadi wa kutolewa kwa mashamba, zile zilikuwa za serikali.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ng'aliot ake bwana commissioner,*

Translator: Inge Bw. Commissioner,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko ng'aliondonon kagimwa ne ba Kwanyi, kitun angwan*

Translator: Ni hii ya mabibi ambao wanaolewa, karibu wanne.

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko uwon kotom koit kamastab Kipsigis missing.*

Translator: Hiyo ijafika sehemu hizi

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Oko tiengei chamet ab chito inegen.*

Translator: Na itategemea vile mtu anavyopenda

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Mayani anyon ale kipitisanjin chito asikoik serikali ne ipitisani, asi kinyokitun kwanyik koik angwan.*

Translator: Sitaki kuwa serikali ndio iwe imeamuru kwamba, mabibi waolewe mpaka

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Amun mami imbaret.*

Translator: Maana mashamba,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Ko ko barien lakwet kwanda komche imbaret*

Translator: Kwa wakati huu tulio nao,

Kipkosgei Arap Chepkwony:*Asigen ano neba kwanyik angwan.*

Translator: Mtoto anapigana, anafanyia vita baba akitaka shamba.

Nitapata wapi shamba ya bibi wanne.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Uwon mayan ng'aliondonono.*

Translator: Neno lingine,

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Ng'aliot ake bwana commissioner,*

Translator: Sikuona ile neno ya kuhusu majimbo, na tulikuwa tumezungumzia

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Ko ng'alek ab Majimbo. Mager en ng'aliondono keng'alalen.*

Translator: Hiyo ingekuwepo, maana itatunza haki za watu mahali walipo.

Kipkosgei Arap Chepkwony: *Kanyalu komi amun, nyalu noton koribon amun ribe kamasta nami.*

Translator: Hayo ndio maneno yangu.

Samuel Kosgei Chepkwony: Asante sana Bw. Commissioner, jina langu ni Samuel Kosgei Chepkwony.

Basi, neno la kwanza Bw. Commissioner, kwa katiba au constitution, inaingilia upande wa land, land issue. Land issue, kwa vile imeteremshwa, serikali, kutoka serikali ya juu, ningeonelea kwamba, ni vizuri, powers iwekwe kwa upande wa village government, serikali ya kijiji. Hili powers wote, wasimamie upande wa shamba, kama mambo ya kuuza, kama mambo ya kudistribute, hapo mahali village, kuna shamba, kwa hivyo kila kijiji iwe na shamba na uwezo kubwa, kuliko kuwa katika locational au kuliko kuwa katika district au regional. Hiyo ni moja.

Ya pili, ni mambo ya citizenship. Application ya mtu ambaye anataka kuwa citizen wa Kenya, ningeonelea ya kwamba ni vizuri, apply, through local authorities, kwa sababu huyu mtu atakuja kuishi ndani ya local, mahali au sisi tumeonelea kwamba, district, kuna district, kuna province, na ile ingine ambaye. Lakini huyu mtu atakuja kuwa katika district. Kwa hivyo ni vizuri, awe, apply through evenvillage, hili ajulikane ataishi wapi, huyo mtu atakuwa mtu wa wapi, na atakuwa mtu wa hiyo area hiyo yote, mahali ambayo amefanya kama district, hiyo atakuwa citizen wa hapo, na atakuwa citizen wa Kenya, kama yule mwenzake mwingine. Hawezi kuwa huko, hakuna shamba huko juu, iko shamba mahali ama Nyumba mahali, iko district.

Ya tatu, ni free education. Free education kwa class ya kwanza mpaka class ya nane, pamoja ya wale ambao disabled, ambao hawajiwezi. Wapatiwe free education, iwe katika katiba, hili hao waweze kufaidika, kama hatuwezi, wazazi wao hatuwezi kwa mambo ya fees, amefika kiwango ya standard 8, anaweza kujitafutia, au kuenda katika upande wa wale ambao wanaweza kukua, kama mwenye bidii, anaweza kuingia katika polytechnic, na anaweza kufanya kazi yake mwenyewe, kama amepata education kidogo kuliko yeye anakaa bila education, yeyote, serikali ijaribu iwe katika katiba.

Hiyo ndio mawaidha, au hiyo ni msemu yangu ya kwamba, ni vizuri huyu disabled, na hawa wengine ambao, primary free education, na anaweza kusaidiwa na serikali. Kwa hivyo hiyo ndio maneno ambayo nilikuwa na tarajia ni kama hayo Bw. Commissioner, asante sana.

Charles Kipruto Saina: *Kigurenon Charles Kipruto arap Saina.*

Translator: Naitwa Charles Kipruto Saina.

Charles Kipruto Saina: *En Katiba ne karager en iyeo, ko kakimwa ng'alek ab commissions.*

Translator: Katika katiba hiyo, nimeona imetaja maneno ya commissions,

Charles Kipruto Saina: *Oko en Katiba ne kokitinye, ngo komakomi anan komi komogigase kechabe abakora commissions.*

Translator: Na katika ile katiba ya zamani, kama ilikuwa imetajwa, ama haikutajwa, tulikuwa tunasikia macommissions nyingi, zilikuwa zikitengenezwa..

Charles Kipruto Saina: *Ko en commissions ichoton tugu l komikasarta ne kikimeto oko katar rabinik.*

Translator: Na katika kazi za macommissions hizo, report zao, hazikuwa zinatolewa, na pesa nyingi zilikuwa zinatumiwa.

Charles Kipruto Saina: *Alelen ingunon en Katiba ini mi kilyanji raini sikobais commission oko katar rabinik ab emet puch.*

